



MUKHTASARI

## Programu ya Pamoja ya Kigoma ya Umoja wa Mataifa

**P**rogramu ya Pamoja ya Kigoma (KJP) ni jitihada inayohusisha mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa (UN) ambayo yamejikita kushughulikia sekta mbalimbali kwa lengo la kuchochea maendeleo katika Mkoa wa Kigoma. Mashirika hayo 16 yanafanya kazi kwa kushirikiana na sekretariati ya mkoa na serikali za wilaya kwa kuzingatia mahitaji ya kimaendeleo ya mkoa na uwezo wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania. Kwa ujumla, programu hii imejikita zaidi katika jamii za wenyeji na pia kwa wakimbizi na wahamiaji.

Mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa nchini Tanzania yanayoshiriki yanashirikiana katika maeneo saba ambayo ni: nishati endelevu na mazingira; uwezesaji vijana na wanawake kiuchumi; kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; elimu kwa wasichana na wanawake vijana; usafi wa maji na mazingira (WASH); kilimo; na, Afya, VVU na UKIMWI na Lishe.

Programu hii ilizinduliwa rasmi mnamo mwezi Septemba, 2017 kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa, washirika wa maendeleo, jamii za wenyeji, wakimbizi na vyama vya kiraia. Programu hii ya pamoja inatekelezwa kwa miaka minne (2017-2021) na ina jumla ya bajeti ya Dola za Marekani milioni 63 ambapo hadi sasa zimepatikana jumla ya Dola za Marekani milioni 22.

### TAASISI SHIRIKI



Empowered lives.  
Resilient nations.



Eneo la 1:

## Kuimarisha upatikanaji wa Nishati Mbadala na Usimamizi wa Mazingira

**E**neo hili linalenga kuimarisha usimamizi endelevu wa mazingira na hatimaye kuchangia katika kutimia kwa lengo la 7 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) linalohusu Nishati Safi na iliyo Nafuu na Lengo la 13 linalohusu Kuchukua Hatua Kukabili Mabadiliko ya Tabia Nchi.

Jitihada katika eneo hili zinalenga yafuatayo:

1. Kukuza uelewa miongoni mwa jamii za wakimbizi na za wenyeji kuhusu masuala ya mazingira, hasa athari za ukataji miti;
2. Kuhamasisha upatikanaji na matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala kwa ajili ya kupikia katika kaya pamoja na kupatikana majiko yenye ufanisi wa kutoharibu mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini; na
3. Kuzisaidia kaya, hasa zile zinazotegemea nishati zinazotokana na mazao ya misitu ili kujipatia riziki, kuanza kutumia vyanzo mbadala hasa katika mnyororo wa thamani wa nishati endelevu za kisasa za kupikia;

Hatua hizi zinasaidiana na shughuli nyingine zinazotekelezwa kupitia maeneo mengine, kwa mfano, Kilimo bora.

### SHIRIKA LINALOONGOZA



**Gerald Runyoro**  
Ofisa Programu wa Taifa  
[G.Runyoro@unido.org](mailto:G.Runyoro@unido.org)

### TAASISI SHIRIKI



Food and Agriculture  
Organization of the  
United Nations



Eneo la 2:

## Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi

**E**neo hili linalenga kuongeza viwango vya kipato vya wanawake na vijana katika mkoa huu na hivyo kuchangia katika kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hasa Lengo la kwanza (Kutokomeza Umaskini) Lengo la tano (Usawa wa Jinsia), Lengo la nane (Kazi zenye Hadhi na Ukuaji wa Uchumi), na Lengo la 9 (Viwanda, Ubunifu na Miundombinu).

Hatua zinazochukuliwa chini ya eneo hili ni pamoja na:

1. Kuimarisha uwezo wa kiuchumi wa wanawake na vijana kwa kuongeza ujuzi;
2. Kuimarisha upatikanaji wa fedha kupitia misaada na mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha na vikundi vya akiba;
3. Kuimarisha miundombinu muhimu ambayo itawasaidia wajasiriamali vijana na wanawake kuimarisha ubora wa bidhaa zao na kupata masoko makubwa Zaidi; na
4. Kusaidia mifumo iliyopo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) inayolenga kuwawezesha vijana, wanawake na makundi ya wanyonge kiuchumi.

Hatua hizi zinaendeleza na kuimarisha juhudi zilizopo katika Halmashauri kuhusu uwezeshaji vijana, wanawake na vikundi vya wenye ulemavu na wanyonge kiuchumi. Eneo hili pia linaendeleza hatua za awali za vyama vya biashara vya wanawake na vituo vya jamii vya vijana.

### SHIRIKA LINALOONGOZA



**Prisca Mgomberi**  
Mtaalamu wa Ufuatiji na  
Programu wa IELD  
[prisca.mgomberi@uncdf.org](mailto:prisca.mgomberi@uncdf.org)

### TAASISI SHIRIKI





Eneo la 3:

## Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto

Lengo la jumla la eneo hili ni kuwawezesha wanawake na watoto kuishi kwa usalama na wakati huohuo kutoa elimu zaidi kuhusu madhara ya ukeketaji na ndoa za utotoni. Hatua za programu zimejikita kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKU-WWA) na kutoa mchango wa moja kwa moja katika kufikia lengo la tano la Malengo ya Maendeleo Endelevu (Usawa wa Jinsia na uwezeshaji Wanawake na Wasichana Wote).

Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) zinawezeshwa kusimamia maeneo ya umma huku elimu kuhusu malezi bora ikitolewa katika kaya kupitia mpango huu. Eneo hili pia linajikita katika kuongeza uwajibikaji katika mifumo ya kisheria ili-yowekwa mahsusi ili kuchukua hatua stahiki na kutoa huduma kwa visa vya ukatili kwa wanawake na watoto.

### SHIRIKA LINALOONGOZA



for every child

**Stephanie Shanler**  
Mtaalamu wa Kinga ya Watoto  
[sshanler@unicef.org](mailto:sshanler@unicef.org)

### TAASISI SHIRIKI





Eneo la 4:

## Kuimarisha elimu ili kuwajengea uwezo wasichana na wanawake vijana

**E**neo hili linalenga kusaidia mamlaka za serikali za mitaa kuongeza uwezo wao wa kutoa elimu bora ya msingi iliyo rasmi na isiyo rasmi, na pia mafunzo ya ufundi, kwa vijana. Pia linalenga kuhakikisha kwamba wasichana wanapata taarifa na msaada kuhusiana na afya ya uzazi kutoka kwa wadau mbalimbali kutoka ndani ya serikali na vyama vya kiraia.

Kupitia hatua hizi, eneo hili linachangia katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hususan Lengo la nne (Elimu Bora na yenye usawa kwa wote na kutoa fursa kwa wote kujiendeleza) na Lengo la tano (Usawa wa Jinsia na uwezeshaji Wanawake na Wasichana Wote).

### SHIRIKA LINALOONGOZA



United Nations  
Educational, Scientific and  
Cultural Organization

**Viola Muhangi Kuhaisa**

Mratibu wa Mradi

[v.muhangi-kuhaisa@unesco.org](mailto:v.muhangi-kuhaisa@unesco.org)

### TAASISI SHIRIKI





Eneo la 5:

## Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira (WASH)

**E**neo la Usafi wa Maji na Mazingira (Water, Sanitation and Hygiene - WASH) linalenga kuzisaidia mamlaka za serikali za mitaa kutoa huduma endelevu.

Huduma ambazo zitahakikisha Maji safi na usafi wa mazingira kwa watu wengi zaidi. Hivyo kuongeza jitihada za upatikanaji wa maji salama ya kunywa kwa jamii, watoto shuleni na katika vituo vya afya.

Miongoni mwa mafanikio yanayotarajiwa kutokana na eneo hili ni kuhakikisha kwamba kipindupindu kinakuwa historia katika Mkoa wa Kigoma. Zaidi ya hayo, utekelezaji wa eneo hili utachangia kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hususan Lengo la 6 la Maji Safi na Usafi wa Mazingira.

SHIRIKA LINALOONGOZA

unicef 

for every child

**Frank Odhiambo**  
Mkuu wa Huduma za Usafi wa  
Maji na Mazingira (WASH)  
[fodhiambo@unicef.org](mailto:fodhiambo@unicef.org)

TAASISI SHIRIKI

unicef   
for every child



World Health  
Organization

UN  HABITAT  
FOR A BETTER URBAN FUTURE



Eneo la 6:

## Kuimarisha sekta ya kilimo na masoko ya bidhaa (Kilimo)

**E**neo hili linalenga kukuza uwezo wa wakulima wadogo wadogo na kuimarisha uwezo wao wa kustahimili na kukabili madhara ya mabadiliko ya tabia nchi. Kwa hiyo, eneo hili limefungamanishwa na Mpango wa II wa Serikali wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP 2) na kuchangia katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), hususan Lengo la 2 la Kumaliza Njaa Kabisa.

Hatua zinazochukuliwa chini ya eneo hili ni pamoja na:

1. Kuongeza uzalishaji kwa kuhamasisha kilimo kinachozingatia tabia nchi na kuongeza maarifa ili kukuza uzalishaji;
2. Kusaidia upatikanaji wa fedha kwa kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha ili kuongeza uwezo wao wa kuwekeza katika kilimo na kupunguza hatari ya wao kupata hasara;
3. Kuimarisha Mnyororo wa Masoko na Miundombinu kwa kuanzisha masoko kupitia vituo vya ukusanyaji na ushirika na sekta binafsi; na
4. Kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno katiika mazao muhimu ya nafaka kupitia hatua kama vile kuanzishwa kwa teknolojia bora zaidi za maghala ya kuhifadha nafaka na kuendeleza teknolojia zinazoongeza thamani kama vile ukoboaji, ukaushaji na usafishaji.

### SHIRIKA LINALOONGOZA



**World Food Programme**

**Kajsa Nyerere**  
Mratibu wa Wakulima  
Wadogowadogo/FTMA  
[kajsa.nyereere@wfp.org](mailto:kajsa.nyereere@wfp.org)

### TAASISI SHIRIKI



**Food and Agriculture  
Organization of the  
United Nations**



**International  
Trade  
Centre**



Eneo la 7:

## Afya, VVU na Lishe (Afya+)

**M**wezi Januari, 2019, Kamati ya Uongozi ya Programu ya Pamoja ya Kigoma ilipitisha Afya+ kuwa eneo la saba la KJP. Mashirika yanayoshiriki katika Afya+ yanashirikiana kwa karibu na sekretariati ya mkoa katika maeneo yafuatayo:

1. Kuimarisha huduma za msingi za kuokoa maisha na utoaji tiba ya afya na VVU kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi;
2. Kuongeza upatikanaji wa matunzo bora, kuimarisha huduma za afya ya uzazi na watoto na za, VVU na lishe;
3. Kukabili woga na unyanyapaa na kuhakikisha kuwa walio hatarini zaidi wanapata huduma za afya kwa wakati, kupitia utoaji taarifa, mafunzo na huduma za rufaa kwenye vituo vya huduma katika jamii zinazohusika; na
4. Kuongeza matumizi ya huduma za afya na lishe miongoni mwa familia na jamii kwa kutoa elimu zaidi na kuhamasisha kuongeza ubora wa huduma kupitia vyombo vya habari.

### SHIRIKA LINALOONGOZA



**World Health Organization**

**Dr. Ritha J. A. Njau**  
Ofisa Mtaalamu wa Taifa  
[njaur@who.int](mailto:njaur@who.int)

### TAASISI SHIRIKI







## Bajeti ya Programu ya Pamoja ya Kigoma

**B**ajeti kuu ya maeneo yote saba ya programu hii ni Dola za Marekani milioni 63, ambapo takribani Dola za Marekani milioni 22 tayari zimepatikana. Mchango mkubwa unatoka katika Serikali ya Norway, ambayo inasaidia maeneo ya Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi (YWEE), Kilimo, Maji Safi na Usafi wa Mazingira (WASH) na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (VAWC). Serikali ya Ireland inachangia kufadhili eneo la Afya+, wakati Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Korea (KOICA) inachangia kufadhili eneo la Elimu kupitia UNESCO. Mashirika yanayoshiriki ya Umoja wa Mataifa pia yamekuwa yakitoa mchango kwa programu hii kupitia fedha za mfuko mkuu ambazo mashirika yanapata kutoka makao yao makuu. Aidha, serikali ya Tanzania inachangia kwenye mradi ikiwa ni pamoja na kutoa wataalamu wanaosimamia utekelezaji na kutoa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa huduma mbalimbali.

Umoja wa Mataifa ungependa kuwashukuru washirika wote, wakiwemo Norway, KOICA, Sweden & Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), kwa kusaidia kifedha programu hii.

### TAASISI SHIRIKI





Norwegian Embassy

**KOICA**  
Korea International  
Cooperation Agency



Sweden  
**Sverige**



**Irish Aid**  
Rialtas na hÉireann  
Government of Ireland

Umoja wa Mataifa unawashukuru washirika wote, wakiwemo Norway, KOICA, Sweden na Shirika la Misaada la Irelanda (Irish Aid), kwa kuisaidia kifedha programu hii.



Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**Evance D. Siangicha**

Mratibu wa Eneo wa Umoja wa Mataifa –

Programu ya Pamoja ya Kigoma

Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa

**Baruapepe:** [evance.siangicha@one.un.org](mailto:evance.siangicha@one.un.org)

**Simu ya mkononi:** +255767800193



# UNITED NATIONS TANZANIA

